# Mtanijengea Nyumba Gani?

Tucson, Arizona USA

Novemba 21, 1965

1 Asante, Ndugu Green. Ni majaliwa. Salamu kwa Ndugu na Dada Green, na wote walio hapa asubuhi ya leo. Na ni majaliwa ambayo ninajisikia nimepewa, kuja mahali hapa pa kuabudia, kutoa matangazo machache.

Sitaki kuchukua wakati wa Ndugu Green hapa, kwa sababu nilimsikia Ndugu Green mara kadhaa, akinena, nami hakika nilishawishika, na kwa kuwa alituletea Neno la Bwana, na ni mnyenyekevu sana juu yake. Jana alisema, "Mimi sipati Neno kutoka kwa Bwana kama labda lingekuja katika ufunuo, kama—kama lilivyotumwa, lakini," kasema, "ninapenda ku—ku kusisitiza juu ya yale yaliyosemwa." Yeye alisema, "Kama vile Paulo alipoandika jambo fulani katika Biblia, naja hapa kusisitiza yale aliyosema." Kasema, "Sina ujumbe, ila kusisitiza tu yale ambayo tayari yamesemwa kutoka kwa Bwana." Sasa hilo lilikuwa la ajabu sana, kijana m—mdogo namna hiyo, na kusema, kutoa matamshi kama hayo.

Sasa hebu na tuwe na maombi pamoja.

2 Mungu mpendwa, ni vigumu kujua jinsi ya kuanza, kwa kuwa ninajisikia Wewe upo hapa leo, na katika Uwepo Wako daima tunajisikia duni sana. Nami ni—ninakushukuru kwa ajili ya majaliwa haya. Sasa, Bwana, ya kwamba Wewe umetupa mahali hapa, tunaomba ya kwamba Wewe utakutana nasi kila wakati tutakapokutana hapa. Na jalia Roho Wako Mkuu atembee juu ya mji huu! Jalia tuweze kuuleta Ujumbe huu wa Injili ambao tumepewa na kukabidhiwa mikononi mwetu katika siku hizi za mwisho, jalia utimizwe, Nawe uipate kila nafsi kutoka Tucson na vitongoji vyake, ambayo Wewe uliikusudia ipate Uzima. Tujalie mambo haya, Baba, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

3 Nafikiri ninataka kusoma kifungu kidogo cha Maandiko hapa asubuhi ya leo, kabla tu sijasema maneno haya ninayotaka kusema. Yanapatikana katika Matendo, mlango wa 7 wa Kitabu cha Matendo. Na wakati mkifungua hapo, tutaanzia kwenye kifungu cha 44.

Sasa tunaenda Shreveport juma hili, juma hili lijalo, kwa ajili ya mfululizo wa ibada, na sasa tutajaribu, Bwana akipenda. Ndugu Moore, Ndugu Jack Moore, rafiki mzuri sana wa mimi na Ndugu Pearry, nasi tunampenda Ndugu Jack. Ujumbe, nafikiri, kwa namna fulani ulimshangaza kidogo, hasa sana juu ya baadhi ya mambo ambayo tunayathamini sana na kuyaamini, ambayo—ambayo yalitujia kwa kule kufunguliwa kwa Mihuri Saba, tunavyoiamini, kama vile, "uzao wa nyoka," na "Usalama wa milele wa waaminio," na—na kadhalika, baadhi ya Jumbe hizo. Hiyo, labda kwa wengine … Hatufikiri Hili ni gumu, lakini, Hilo, huna budi kuufungua moyo wako kwa ajili ya Kweli. Tunaamini ya kwamba tunaishi katika wa—wakati wa mwisho. Hiyo ni halisi sana kwetu, ya kwamba tuko tu mwisho wa safari.

4 Na kuhubiri katika kanisa la mtu mwingine, vema, unataka kuuheshimu ukarimu wa mtu huyo, wa—wa kukupa nafasi hiyo ya kuja kanisani mwake. Nami, bila shaka, nikijua ya kwamba hawaamini jambo Hilo, nami ningewaheshimu vya kutosha kwamba … Kuna mengi zaidi ninayoweza kuhubiri huko, mbali na kuuingiza Huo ndani; isipokuwa iwe ni Roho Mtakatifu anausukuma Huo kidogo, mnaona, basi bila shaka ningesema kama alivyosema Yeye. Wala sijui lingine ila kufanya hivyo, nami natumaini kamwe sitajifunza vema zaidi ya kufanya hivyo. Mnaona? Hebu na tuliseme tu jinsi anavyolisema.

5 Sasa hebu na tusome tu a—aya moja ama mbili hapa kutoka kwenye—kwenye sura ya 7 ya Kitabu cha Matendo, kuanzia kifungu cha 44.

> *Ile hema ya ushahidi ilikuwa pamoja na baba zetu jangwani, kama alivyoagiza yeye aliyesema na Musa, ya kwamba aifanye sawasawa na mfano ule aliouona;*
>
> *Ambayo baba zetu, kwa kupokezana, wakaiingiza pamoja na Yoshua katika milki ya Mataifa wale, ambao Mungu aliwafukuza mbele ya baba zetu, mpaka siku za Daudi;*
>
> *Aliyepata fadhili mbele za Mungu, naye aliomba ampatie Mungu wa Yakobo maskani.*
>
> *Lakini Sulemani alimjengea nyumba.*
>
> *Ila Yeye aliye juu hakai katika nyumba zilizofanywa kwa mikono, kama vile asemavyo nabii,*
>
> *Mbingu ni kiti changu cha enzi, . . . na nchi ni pa kuwekea miguu yangu; Ni nyumba gani mtakayonijengea? Asema Bwana: au ni mahali gani nitakapostarehe?*
>
> *Si mkono wangu uliofanya haya yote?*

6 Juu ya Hili, kusomwa kwa Andiko hili, ninataka kusema maneno machache ninayotaka kusema kabla ya Ndugu Pearry kuleta ujumbe wa asubuhi.

Ninaona huu ni mmoja wa nyakati kuu sana za kuzuru kwangu Tucson. Nilikuja hapa kwa sababu niliongozwa kuja hapa. Nimekuja hapa kwa sababu Roho Mtakatifu, kupitia ono, alinituma hapa. Ninajua

hilo huenda likaonekana ni la ajabu, labda. Lakini Yeye, kadiri nijuavyo mimi, cho chote nijuacho juu ya Mungu, nilitumwa kwa ono huko Tucson. Nimeshangaa jinsi nilivyopata kutumwa mahali hapa pa jangwa. Na halafu hapa ambapo kuna …

Nikizungumza kiroho, juu ya mji huu, sijui mahali popote palipo na wafu kiroho zaidi, kuliko katika mji wa Tucson. Kuna vita kati ya makanisa. Kuna mizozo kati ya makusanyiko. Hakuna umoja, na kila mtu akinyakua, na kushikilia, na kufinya, na kujaribu kumpata *huyu*, na kugeuza watu. Ni jangwa, tukinena kiroho, pia.

7 Lakini hata hivyo nilisoma katika Biblia, ambapo Mungu alimwita Musa awaache wapendwa wake na yote aliyopenda, na kumtuma nyikani, apate kuziandika Torati za Biblia. Hilo lilikuwa ni Agano la Kale, Vitabu vinne vya kwanza, Mwanzo, Mambo ya Walawi, na Kumbukumbu la Torati, Kutoka. Yeye … Kamwe sikuvitaja jinsi vinavyofuatana, bali hivyo ni Vitabu vinne. Hilo kweli ndilo Agano la Kale. Kwa sababu, hivyo vilivyobakia vilikuwa ni yale waliyosema manabii, katika Zaburi za Daudi, na kadhalika, bali Mambo ya Nyakati ya wafalme. Lakini hii ilikuwa ndiyo misingi ya Agano la Kale. Je! Musa aliviandika baada ya kuitwa atoke kwenye nchi ya uenyeji wake, ambako alizaliwa na kukuzwa miongoni mwa watu wake, naye akatumwa jangwani, kuandika Kitabu hiki cha Agano la Kale.

8 Ndipo ninaona jambo hilo katika Kitabu cha Agano Jipya, ambapo Paulo, ambaye ndiye mwandishi, ama si mwandishi, bali mwandishi wa Agano Jipya. Pia yeye aliondolewa miongoni mwa watu wake, na, kwa Roho, akaenda Uarabuni, ambako alikuwa kwa muda wa miaka mitatu na nusu, apate uvuvio. Na Paulo ndiye mwandishi mkuu wa Agano Jipya. Sasa, kuna Mathayo, Marko, Luka, na Yohana, bali walikuwa waandishi walioandika tu yale Yesu aliyosema walipomfuata. Na, lakini, ukikichukua Kitabu cha Timotheo, na kwa Warumi, na kwa Waebrania, na kadhalika, Paulo alipokea uvuvio kuliandika Agano Jipya; akilichukua Agano lote la Kale kama kivuli, na kuliweka katika utaratibu. Naye Mungu akaliheshimu, na kulifanya Agano Jipya.

9 Na sasa ikiwa ilibidi Agano la Kale liondolewe kutoka kwa ninii…ilibidi mwandishi huyo aondolewe kwa watu wake, aingie nyikani, apate uvuvio wa kuandika Agano la Kale. Na katika Agano Jipya, aliyeliandika aliongozwa na Mwandishi, akapelekwa mahali pa jangwa, apate uvuvio wa kuliandika Agano Jipya. Na vile Vitabu vimetiwa muhuri kwa Mihuri Saba; pia ingehitaji jambo lile lile, ninaamini, katika siku hizi, kufungua ile Mihuri Saba. Kuacha yale unayothamini, yale unayopenda sana, na makazi madogo niliyopewa na watu, na miongoni mwa watu wangu wote na marafiki, na kanisa lililokuwa likisitawi, wala halikupungukiwa na kitu; na ku—kuyaacha hayo, kujiondoa kwake, na kuhama, kuingia katika jangwa ambako hukumjua mtu, na kila kitu kinakupinga.

Lakini kuna jambo fulani kumhusu Mungu, ya kwamba Yeye humsukuma mtu kufanya mambo ambayo yamepita mawazo yake yote, kusudi yawe ni kwa ajili ya utukufu na heshima ya Mungu. Nami ninajisikia ya kwamba, sio kwa kujiheshimu, bali na—naona ilikuwa ni baraka kuacha kila kitu nilichopenda, kuhamia huku kwenye nyika hii na kuteseka jinsi ambavyo sijawahi kuteseka maishani mwangu, hapa kwenye nyika hii, ama jangwa hili. Lakini ninaamini, ya kwamba katika kufanya jambo hilo na kutii yale Mungu aliyoamuru yatendeke, Mungu ametufungulia siri za siku hii ya mwisho. Nasi tuko hapa na Ujumbe huu.

10 Sasa, kulikuwa na watu wengi walionifuata, na hilo si jambo la kawaida. Kwa kawaida mtu tunayeninii… Watu wanapendana, nao huo, upendo, utakusukuma kufanya mambo usiyowazia ungeyafanya. Na wengi wenu mliyaacha makazi yenu, mliacha yote, kwenda tu, mje huku jangwani.

Wengi wamenipigia simu, wengi wameniuliza, "Twende Arizona? Pangekuwa ni mahali pazuri kwetu?" Vema, kama ilivyosemwa juu ya Musa na hao wengine, hapakuwa ni mahali pa tunda, si mahali pa komamanga.

Hapa hakuna kazi nyingi za kufanya, na maisha ni ya juu, na gharama ya maisha ni kubwa. Kwa kweli ni mahali pagumu pa kuishi, huku Tucson, Arizona; mishahara ni duni, na—na chakula ni ghali, na kodi ya nyumba. Ni—ni mahali pa kutisha sana kuishi, kwa namna hiyo. Bali ni pazuri kiafya, ni pakavu. Nasi wakati mwingine … Haitupasi kufanya nia zetu zifanane na mambo ya dunia hii.

11 Hatuna budi kuutazamia uongozi wa Roho Mtakatifu. Lakini jambo moja lililonisumbua katika kuja hapa, na kuwaambia watu, vema, "hupaswi kuja" ama "unapaswa kuja," ambalo ninamwachia kila mtu binafsi, jinsi Mungu anavyomwongoza mtu huyo kufanya. Nafikiri kila mmoja wetu anapaswa kufanya hivyo, aongozwe na Roho, juu ya la kufanya.

Na wengi wenu hapa wanatoka Jeffersonville, na wa kusanyiko pale, nanyi mmekuja hapa. Sasa, jambo lililonisumbua, lilikuwa ni mahali pa kuabudia.

Nami ninatambua, kama nilivyosoma katika Maandiko hapa, juu ya Stefano na hotuba yake kabla tu ya kifo chake; kwa kuwa walimpiga mawe mara baadaye, kwa ajili ya ujumbe wake. Alipokuwa akinena, alisema, "baba zetu," akinena juu ya Waebrania katika siku za mwanzoni, jinsi walivyojaribu kupata kibali mbele za Mungu, kujenga mahali pa kuabudia. Yeye alisema ya kwamba, "Sulemani alimjengea nyumba,

ama jengo." Tunaijua hadithi hiyo.

12 Lakini ninapenda maneno yake yafuatayo, "Lakini Yeye Aliye juu sana haishi katika nyumba zilizojengwa kwa mikono," na mahali pengine katika Isaya. Yeye alisema, "'Umeniandalia mwili; mnaona, dhabihu na sadaka, na mijengo, na kadhalika, bali umeniandalia Mimi mwili.'" Vema, tunatambua ya kwamba alikuwa akinena juu ya ule mwili ambapo Mungu alifanya maskani yake, katika Kristo.

Lakini ninaamini siku hizi, ya kwamba uvuvio ambao umemjia nanii—Ndugu Green, kuhamia hapa, yeye na Dada Green, wakayaacha makazi yao huko mashariki, tena, pia, huko Texas, kuja hapa pamoja na… kuanza bila kitu; kwa uvuvio tu, wakijisikia ya kwamba wanapaswa kufanya hivyo. Ninawathamini watu watakaoufuata mwongozo wa Kristo, haidhuru gharama itakayowagharimu.

13 Ingawa ulimwengu mzima, labda marafiki wako wa karibu sana, wanafikiri ya kwamba umekosea, bali si kosa kwako. Mradi tu unajisikia kuna kitu fulani nyuma yake, ni Mungu akikuogoza; kamwe haikosei, na daima itatokea vizuri.

Mwone mume na mke hawa vijana, kijana mwanamume mwenye kipaji. Mimi sisemi jambo hili kwa sababu ameketi hapa. Na mama huyu mdogo pamoja na watoto wake wachanga, akiwa na familia ya kulea, naye ameiacha kazi yake na kila kitu, kuja hapa.

Ninatambua ya kwamba miaka mingi iliyopita niliitwa katika huduma. Kamwe sijawahi kuwa mchungaji aliyefanikiwa, kwa sababu nina roho ya kutangatanga, na kurandaranda. Siwezi kuridhika popote. Po pote tu Roho aendapo, sina budi kuambatana Naye, kwa sababu nina Ujumbe. Yesu alisema, "Sina budi kuhubiri katika mji huu mwingine pia."

14 Lakini kuna wale ambao ni wachungaji wanaolichunga kundi. Ninashukuru sana kwamba Ndugu Pearry alifuata uongozi wa Roho Mtakatifu, na leo tuna maskani. Ni dogo. Hilo ni zuri tu la kutosha kwanza, kuona kile Roho Mtakatifu … Bila kujua, hebu na tusogee hatua kwa hatua. Sasa, ninaamini, kama Mungu amezungumza na Ndugu na Dada Green, waje hapa, na amefungua mahali ambapo watoto wetu; badala ya Jumapili asubuhi kuendesha baiskeli zao, na mitaani na kuzurura, wana mahali pa kuja kuabudu, badala ya sisi kuketi huku na kusikiliza kitu ambacho tumesikia kwenye redio, ambacho ni sawa.

15 Lakini sisi, kama kundi hili la watu, tuna Ujumbe kwa ajili ya siku hii. Sisi, tunaamini ya kwamba Mungu ametupa Ujumbe. Na Ndugu Green, ni, sitaki kumwita mshirika wangu, kwa sababu sisi … Vema, ndivyo alivyo, pia, mshirika wangu, tuko pamoja katika Ujumbe huu. Ndugu Green huhubiri jambo lile lile pamoja na Ujumbe ninaoamini. Ameondoka nyumbani mwake, amewaacha watu wake, ameacha kanisa lake. Alikuwa, ninaamini, alikuwa mkuu wa jimbo ama kitu kama hicho, wa moja ya mashirika hayo, naye akakiacha kitu hicho chote alipousikia Huu. Aliacha kila kitu alichokuwa akikipenda, pia, kuja jangwani, kuunga mkono tu kile Mungu anachotupatia sasa.

16 Ninasema si kwamba tu anapaswa kuwa mioyoni mwetu, inapaswa kuwa ni jukumu letu kumuunga mkono, kila tuwezacho, kuzihudhuria ibada, kuja hapa kuabudu, na kupafanya mahali hapa kuwa mahali ambapo Mungu anaweza kutufunulia mambo aliyo nayo ya kutufunulia. Na kama neno Lake lilivyosema, "Ujumbe haunijii mimi kwa kutolewa kwa uvuvio, kama unavyofanya kwa labda baadhi yetu, lakini," yeye alisema, "Nipo hapa kuunga mkono kile Mungu ametoa." Ni tamshi lililoje! Nami ninaamini, kama sote tutashirikiana pamoja, tutaiweka mioyo yetu kwa hilo.

17 Ninajua ya kwamba kila mmoja wenu, kama mkijisikia kama ninavyojisikia, nina njaa sana kumwona Roho wa Mungu akitenda kazi, ni vigumu kwangu kuvumilia jambo hilo. Matukio fulani ambayo ndiyo kwanza niyapate huko mlimani, kujisikia tu ya kwamba mara nyingine tena, kile kitu Fulani ambacho wakati nilipookoka kwa mara ya kwanza kilikuwa ni cha ajabu sana moyoni mwangu! Nasi tunaweza kufikia mahali, tunaweza kuketi na kukiona miongoni mwetu, ya kwamba tunakauka. Tunapoketi hapa jangwani, ninakutana na ndugu zangu, wanazungumza nami na ninazungumza nao; daima, kwa njia ndogo ya kuangalia, kuhisi huko nje na Roho, kama ilivyokuwa, kuona tu hali ya ndugu huyo, kuona kuna shida gani. Naanza kuhisi sisi sote tukitandawaa, tukimwacha Roho. Limekuwa ni jambo la kawaida sana kwetu. Hatuna budi kuabudu katika Roho, ambapo Roho wa Mungu … Si tu Ujumbe wetu unapaswa kuwa mwali wa wakati huu, unapaswa kuwa ni mwali mioyoni mwetu. Mnaona? Halina budi kuwa mioyoni mwetu, ama hatuwezi—hatuwezi kulionyesha kwa watu. Roho hana budi kuubeba Ujumbe, Mwenyewe. Nami ninamtumaini na kumwamini kila mmoja wenu, kuwa Mkristo halisi.

18 Sasa wanahitaji waalimu wa shule ya Jumapili. Watahitaji watumishi. Nami nataka kusema jambo hili kusudi mpate kufahamu kabisa. Hili ni kanisa langu.

Nimekuwa hapa miaka mitatu. Nami nimekuwa na mlango mmoja uliofunguliwa kwangu, huo ulikuwa Ndugu Mack aliniomba nije nihubiri. Mungu ambariki. Sijaalikwa na watu wengine wowote; Hakuna kitu dhidi yao, wako sawa. Ndugu Brock, rafiki yangu mzuri, Ndugu Gilmore, wengi wa hawa ndugu wa Kipentekoste hapa, ni marafiki zangu wazuri sana. Ninawapenda; hakuna kitu dhidi yao. Ninaelewa msimamo wao. Hawawezi kunialika mle ndani, kisha wabaki katika madhehebu yao. Mnaona, hawawezi

kufanya hivyo. Kwa sababu, wakifanya hivyo, wanafukuzwa. Kwa hiyo mnaona msimamo wao. Nilikuwa na jambo lile lile la kukabiliana nalo. Lakini, jamani, na iwe daima, "Utafuteni kwanza Ufalme wa Mungu," mapenzi ya Mungu.

19 Na sasa kwa kuwa, Ndugu Green, Mungu amemtuma humu na kutufungulia kanisa lenye Imani ya thamani kama ile tunayoiamini, inatupasa kumshukuru sana Mungu, na kuhudhuria kila ibada, kuchukua kila mahali tuwezapo. Na kama tukiombwa kuomba, kuomba, kutafuta, kufanya, hebu tuwe askari moja kwa moja kwenye … tu wenye shauku ya kufanya jambo hilo. Mnaona?

Dumisha Ujumbe kwa heshima, na uishi maisha mazuri. Msiache uchafu wowote uje juu Yake. Tunaishi ambapo wakati umeenda sana sasa. Tume—tumechelewa sana kwenye majira. Hebu tuishi yaliyo safi. Vema, maisha yangu, maisha yako, maisha yetu yote yanahitaji kunyanyuliwa, mbele za Mungu.

Vijana wetu wanaendesha tu kila mahali, kutoka mahali hadi pengine, kutoka kwenye tamasha moja hadi lingine, wakizidi kuelea mbali zaidi na zaidi mbali na Mungu. Sawa. Sasa, hiyo ni kweli. Ninaona jambo hilo katika watoto wangu, nami ninajiona ninafikia mahali ambapo si … Ninyi, hamna bdui tukutane pamoja, kumwabudu Mungu; Biblia ilisema hivyo, "Tunapoiona siku hii ikikaribia, zaidi sana tukusanyike pamoja." Kama kuna watu wawili tu hapa, wewe uwe mmoja wao. Sasa hiyo ni … Na kama tukikusanyika pamoja na kuabudu pamoja, basi tunaninii tu, jambo fulani juu ya jambo hilo, Yesu alisema, "Walipo wawili watatu wamekusanyika katika Jina Langu, mimi nipo hapo miongoni mwao."

20 Sasa, kama nilivyosema hapo awali, Ndugu Green aliniambia, naye akalisema. Mke wangu alikuja, akaniambia yale aliyosema nilipokuwa mbali. Hilo, naye alisema asubuhi ya leo, "Mimbara ilikuwa wazi wakati wo wote." Sasa kwa kawaida … Hiyo ni, imefunguliwa kwa ajili ya mimi kuhubiri.

Sasa, kwa kawaida, ilinibidi kuendesha gari kote mpaka Jeffersonville, Indiana, kuutoa Ujumbe ambao Mungu alinipa, kuwaletea watu; kwenda kote mpaka Jeffersonville, Indiana, na kila mmoja wenu akijiunganisha kote nchini, na kujiunganisha kwa simu na kadhalika, kuupata Ujumbe, kwa sababu huo ndio tunaoishia. Mnaona, hilo ndilo lililotuleta hapa. Vema, haitubidi kufanya hivyo tena.

21 Mungu hunipa Ujumbe, ninaweza kuja papa hapa mimbarani na kuuhubiri, na kujisikia huru kufanya hivyo. Naam. Nami ninaamini, kwa jambo hilo, ya kwamba Mungu Mwenyezi atawabariki kama mkisimama tu na kanisa hili sasa, kundi hili la watu. Si hivyo tu, bali hebu na tutoke tuone kama hatuwezi kuwafanya wengine waingie. Mnaona, hebu tuzungumze na wengine kila mahali, tuzungumze nao kuhusu kanisa letu na maana yake. Kile kanisa letu … Tuko hapa. Tunawatakeni mje, mkawalete wageni, nami nina hakika itakuwa vizuri kwetu sote. Mnaona? Tuna jengo, ambalo tunazo shukurani kwa ajili yake. Tunashukuru kwa ajili ya mahali hapa, kukusanyika pamoja.

Lakini, "Ila Yeye aliye juu hakai katika nyumba zilizofanywa kwa mikono, mnaona, 'Kwa kuwa Mbingu ni kiti Changu cha enzi, na nchi ni pa kuwekea miguu Yangu; na ni mahali gani nitakapostarehe? Lakini Wewe umeniandalia mwili.'"

Nasi ni Mwili wa Kristo. Kwa hiyo tunapoondoka kutoka kwenye jengo moja hadi kwenye jengo jingine, ninaamini, katika kuleta Jumbe zetu, nasi tutashuka na kufanya ibada za uponyaji. Na cho chote kile Bwana atakachotufunulia kufanya, tutakuwa nacho papa hapa kanisani, mpaka kitakapokuwa kimejaa sana itakubidi kukipeleka mahali pengine, na mahali pengine, mpaka Yesu atakapokuja. Mungu akubariki.

22 [Ndugu Pearry Green anatoa maoni yake, halafu anamwomba Ndugu Branham kumweka wakfu. Sehemu tupu kwenye kanda — Mh.]

Na tuinamishe vichwa vyetu.

Mungu mpendwa, tunaposimama hapa kwenye jukwaa hili, ambalo linawakilisha, moja kwa moja hapa madhabahuni, tunatambua ya kwamba sisi ni ja—jamii ya watu wanaokufa, kuhusu mambo ya dunia hii. Tunaangalia mitaani na kuona dhambi imeandikwa kila mahali, na kwamba Utukufu wa Bwana unaondoka upesi. Nasi tunajua, wakati Utukufu wa Bwana utakapopaa juu, vivyo hivyo Kanisa litaambatana Nao. Mungu, tunataka kuwa kule.

Siku chache tu zilizopita, nikisimama hapa pembeni mwa barabara, ng'ambo tu ya barabara, nikiangalia lile gwaride likishuka kwenda barabarani; na nikiviona hivyo vifaru vya kale vya Vita Vya Kwanza vikiongoza, ndipo kikaja kifaru kikubwa na kizito cha Sherman, nyuma ya hicho vikafuata na kufuatana, kisha akina mama wenye nyota za dhahabu; maskini familia ndogo iliyovunjika, huku mke analia, na maskini mvulana mdogo mwenye matambara aliyempoteza baba yake, maskini mama kizee alikuwa amempoteza mwanawe. Nikawaza, "Ni huzuni jinsi gani," kusimama pembeni mwa barabara na kuangalia kitu kama hicho kikipita. Kisha kuona, mara tu walipolipita jengo hili, muziki ukabadilika ukawa, *Twendeni, Askari Wakristo*. Wakipiga hatua zao taratibu, nyuma; bali walipopita mahali hapa!

23 Mungu mpenzi, ninawazia juu ya wakati mwingine mkuu unaokuja, na huo utakuwa ni ufufuo, wakati watu wa kale watakapotokea kwanza, watakatifu, wale wazee wetu. "Kwa maana sisi tulio hai, tuliosalia,

hatutawatangulia wala kuwazuia hao waliokwisha kulala; kwa kuwa baragumu ya Mungu italia, nao waliokufa katika Kristo watafufuka kwanza." Ndipo tunapoona jambo hilo kuu … ni watu tu wanaokwenda, wakitembea juu angani; nasi tutasimama, tukingojea badiliko letu, tukijua ya kwamba tutaingia mstarini, pia. Mungu, tufanye askari waaminifu.

Ni wale tu ambao kwa kweli wamehusika na wamekuwa vitani ndio wangejua maana ya jambo hilo kwa kweli, kuona vifaru hivyo vikivingirika hapo. Na, Mungu, tunafikiri ya kwamba wale ambao wamekuwa katika vita vya uzima watajua maana yake, tunapongojea zamu yetu kuingia mstarini na mahali petu, katika ule ufufuo, kupaa juu.

24 Na huyu, ndugu yangu mdogo, anayesimama hapa, amefunzwa vizuri, yuko tayari, amevaa nguo, akingojea mzee kumwekea mikono, mzee shujaa anayetoka pale kwenye mstari wa mbele wa vita, akijua ya kwamba hana budi kuingia vitani, pia. Mungu mpendwa, kwa mikono hii isiyostahili niliyoiweka juu ya ndugu yangu, ikiiwakilisha Yako. Mbariki Ndugu Green, Mungu mpendwa, ambaye ninambariki katika Jina la Yesu. Jalia auchukue Ujumbe huu, Bwana, katika mji huu na popote utakapomwita. Jalia awe mwaminifu, aliyejazwa na Roho, akiishi maisha yasiyo na lawama. Mungu, jalia aihurumie mioyo ya watu, apate kuwafundisha na kuwaongoza na kuwaelekeza kwenye njia ambayo sote tunatamani kuipitia. Tujalie, Bwana.

Mbariki mke wake mwaminifu, watoto wake wadogo. Bariki juhudi zetu hapa pamoja, kama ndugu Wakristo hapa duniani, tupate kuipeleka Injili hii hata miisho ya dunia. Tuma Roho Wako juu yake, Mungu. Tunaomba katika Jina la Yesu Kristo, tunapomtoa Kwako. Amina.

Mungu akubariki, Ndugu Pearry. Beba Neno la Mungu!

MESSAGE hub online
www.messagehub.info

Mahubiri Na
William Marrion Branham
"... katika siku za sauti ..." Ufu. 10:7